TANGAZO LA SERIKALI NA. 871 la tarehe 18/10/2024

SHERIA YA CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA,
(SURA YA 315)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 14(1))*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA MITIHANI ZA CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA, 2024

Jina
TS Na. 927 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Mitihani za Chuo cha Elimu ya Biashara za mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Mitihani za Chuo cha Elimu ya Biashara za mwaka 2023, ambazo zitajulikana kama Kanuni Kuu.

2. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa ujumla kwa-
(a) kufuta neno "NACTVET" popote linapotokea na badala yake kuweka maneno "Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi";
(b) kufuta neno "NTA" popote linapotokea na badala yake kuweka maneno "Tuzo ya Kitaifa ya Ufundi"; na
(c) kufuta neno "TCU" na badala yake kuweka maneno "Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania."

Marekebisho ya kanuni ya 3

3. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kufuta tafsiri ya neno "utoro" na badala yake kuweka tafsiri ifuatayo:

"utoro" maana yake ni kutofanya mtihani uliopangwa, au kushindwa kuhudhuria masomo yaliyopangwa kwa asilimia inayotakiwa au kushindwa kuahirisha masomo bila sababu ya msingi ambayo itatolewa ushahidi.

Marekebisho ya kanuni

4. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 14

ya 14

kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (12) yafuatayo:

"(13) Mwanafunzi ambaye hajaridhika na mwenendo au tathmini ya tathmini endelevu katika moduli -

(a) ataripoti suala hilo kwa maandishi ndani ya siku tano, kwa mwalimu wa moduli husika kwa utatuzi wa wakati;

(b) endapo mwanafunzi hajaridhika na uamuzi wa mwalimu wa moduli au suala hilo halijatatuliwa na mwalimu wa moduli ndani ya siku saba tangu tarehe ya kuripoti suala hilo, mwanafunzi ataripoti suala hilo kwa maandishi ndani ya siku tano kwa Mkuu wa Idara husika;

(c) endapo mwanafunzi hajaridhika na uamuzi wa Mkuu wa Idara au suala hilo halijatatuliwa na Mkuu wa Idara ndani ya siku saba, mwanafunzi ataripoti suala hilo kwa maandishi ndani ya siku tano kwa Naibu Mkuu wa Chuo - Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu kwa uamuzi wa mwisho.".

Marekebisho ya kanuni ya 18

5. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 18 kwa kuongeza mara tu baada ya kanuni ndogo ya (8) yafuatayo:

"(9) Mwanafunzi ambaye hajaridhika na mwenendo wa mafunzo kwa vitendo, projekti, utafiti au tasnifu-

(a) ataripoti,kwa maandishi ,ndani ya siku tano kwa msimamizi husika kwa ajili ya utatuzi ndani ya wakati;

(b) endapo mwanafunzi hajaridhika na uamuzi wa msimamizi au msimamizi ameshindwa kutatua suala hilo ndani ya siku saba tangu tarehe ya kuripoti suala hilo, mwanafunzi ataripoti suala hilo kwa maandishi ndani ya siku tano

kwa Mkuu wa Idara husika;

(c) endapo mwanafunzi hajaridhika na uamuzi wa Mkuu wa Idara au Mkuu wa Idara ameshindwa kutatua suala hilo ndani ya siku saba, mwanafunzi ataripoti suala hilo kwa maandishi ndani ya siku tano kwa Naibu Mkuu wa Chuo - Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu kwa uamuzi wa mwisho.”.

Marekebisho ya kanuni ya 30

6. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 30 kwa kuongeza mara tu baada ya kanuni ndogo ya (19) yafuatayo:

“(20) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (18), mwanafunzi anaweza kuomba kwa maandishi ndani ya siku tano tangu tarehe ya uamuzi wa upande mmoja kutengua uamuzi huo, iwapo atairidhisha Kamati ya Kushughulikia Ukiukaji wa Taratibu za Mitihani kwamba kulikuwa na sababu za msingi za kutofika.

(21) Kamati ya Kushughulikia Ukiukaji wa Taratibu za Mitihani baada ya kuridhika na maombi yaliyofanywa chini ya kanuni ndogo ya (20), itatoa amri ya kutengua uamuzi huo na kupanga siku ya kusikiliza shauri hilo.”.

Marekebisho ya kanuni ya 32

7. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 32 kwa kufuta kanuni ndogo ya (6).

Marekebisho ya kanuni ya 45

8. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 45 kwa-

(a) kufuta kanuni ndogo ya (1);

(b) kupanga upya kanuni ndogo za (2), (3), (4) na (5) kama kanuni ndogo za (1), (2), (3) na (4) mtawalia;

(c) kufuta kanuni ndogo ya (4) kama ilivyopangwa upya na badala yake kuweka yafuatayo:

“(4) Isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo na Naibu Mkuu wa Chuo - Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu, rufaa

itawasilishwa kwa ofisi ya mitihani kupitia mfumo wa taarifa za wanafunzi baada ya kulipwa kwa ada husika."

(d) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (4) kama ilivyopangwa upya yafuatayo:

"(5) Kamati ya Rufaa ya Matokeo ya Mitihani itaamua rufaa hiyo ndani ya siku ishirini na moja baada ya kumalizika kwa muda wa rufaa; na

(6) Masharti ya kanuni hii hayatatumika kwa masuala yaliyoelezwa chini ya kanuni ya 14 na 18.".

Dar es Salaam,
10 Oktoba, 2024

WINEASTER S. ANDERSON
*Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi*

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA · WELEDI NA UBORA · PROFESSIONALISM & EXCELLENCE · THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA